# NSSF sasa yaingia kidigitali

**Na Salome Kitomari**

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), limefanya mabadiliko katika mfumo wa mawasiliano kwa kuanza utaratibu wa kidigitali katika kutoa na kupokea taarifa kutoka kwa wanachama na wastaafu.

Meneja Kiongozi wa Uhusiano na Elimu kwa Umma wa NSSF, Lulu Mengele (pichani juu), alisema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi na kueleza kuwa mabadiliko hayo yanalenga kuhakikisha wanachama wanapata taarifa zote muhimu kwa wakati kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama).

"Huduma hii ni kwa wanachama na wadau wote kwamba wanaweza kupata taarifa zote muhimu, kuuliza na kujibiwa kupitia njia za Tehama. Wastaafu wanaweza kuuliza taarifa zao mbalimbali ambazo ni muhimu kwao," alisema.

Aidha, alisema mfumo huo utajikita katika kushughulikia malalamiko, maulizo na maoni ya wanachama wake na wadau wengine wa shirika, lengo likiwa kuwafikia kwa haraka na kupunguza usumbufu.

Kwa mujibu wa Meneja huyo, wanachama na wadau hao watapiga simu bure kuanzia saa 2:30 asubuhi hadi 10:30 jioni kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa na watoa huduma watakuwa tayari wakati wowote kutatua changamoto walizo nazo au kutoa elimu.

Mengele alisema shirika hilo litaendelea kuboresha mifumo yake ya mawasiliano na utendaji ili kuhakikisha huduma zote muhimu zinawafikia walengwa kwa wakati.

NSSF ni mfuko wa hifadhi ya jamii unaohudumia wanachama wa sekta binafsi ambao kikokotoo cha mafao yake ni asilimia 25 ya mkupuo baada ya mwanachama kustaafu na asilimia 75 utalipwa kama mshahara kwa kipindi chote cha maisha yake.

Aidha, katika mfuko huo kuna fao la upotevu wa ajira lililoanzishwa na Sheria ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2018, ambayo inaelekeza mwanachama kulipwa asilimia 33.3 ya mshahara wake kwa kipindi cha miezi sita akiwa anatafuta kazi nyingine na anapokosa atatakiwa kumjulisha Mkurugenzi wa mfuko michango yake kuhamishiwa kwenye fao la hiari.